




JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA CHEMBA  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)



FAX/ SIMU: 0262360175  
E – MAIL: [ded@chembadc.go.tz](mailto:ded@chembadc.go.tz)

S.L.P 830  
CHEMBA

Kumb. Na. CDC/L.20/7 VOL.I /23

15/03/2022

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MUDA YA KUKUSANYA TAARIFA  
ZA ANWANI YA MAKAZI NA POSTIKODI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba anapenda kuwatawagazia wananchi wote wenye sifa nafasi 120 za maombi ya ajira ya muda kwa kazi ya kuandika namba, kukusanya taarifa kwenye zoezi la anwani za makazi na kui ngiza katika mfumo katika kata, Vijiji na Vitongoji vyote katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

**A. SIFA ZA WAOMBAJI**

- i) Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18-35.
- ii) Awe na elimu kuanzia kidato cha nne na kuendelea.
- iii) Awe anamiliki simu janja yenye Android yenye uwezo wa kukaa na chaji siku nzima.
- iv) Awe na barua pepe (Email address) na nywila (Password) inayofanya kazi.
- v) Awe na uwezo wa kusoma ramani za Vijiji.
- vi) Awe ni mkazi wa Kata husika katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.
- vii) Awe na kitambulisho cha NIDA.
- viii) Asiwe mtumishi wa Umma.

**B. KAZI NA MAJUKUMU**

- a) Kugawa/kuandika namba za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma za jamii.
- b) Kukusanya taarifa za nyumba, viwanja na maeneo ya huduma za jamii kwa kutumia simu janja yenye Android.
- c) Kukusanya taarifa za wamiliki wa nyumba, viwanja na maeneo ya huduma za jamii kwa kutumia mfumo wa Anwani za Makazi.
- d) Kutuma data kwenye mfumo wa Anwani za Makazi.
- e) Malipo kwa mwezi ni shilingi laki sita (Tshs. 600,000).

**C. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA:**

1. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na kuendelea iliyothibitishwa na Kamishna wa viapo.
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa iliyothibitishwa na Kamishna wa viapo
3. Picha (Passportsize 2).
4. Barua ya maombi ipitie kwa Mtendaji wa Kijiji anapoishi muombaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Chemba.

**D. JINSI YA KUTUMA MAOMBI**


Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji, ya simu, barua pepe(E-mail) na ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi wa Mtendaji kwa anwani ifuatayo;

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
S.L.P 830  
CHEMBA

**E. TAREHE YA MWISHO YA KUPOKEA MAOMBI**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/03/2022 saa 9.30 Alasiri

Limetolewa na:

  
Siwema Hamoud Jumaa  
MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
CHEMBA

MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA  
CHEMBA